# AMINA LAIZER:

# Mama anayeishi ndoto za Rais Ravalomanana na biashara ya maziwa

NA WARIOBA IGOMBE

KATIKA maisha, mara nyingi binadamu tunategemeana hasa kwenye suala zima la kutafuta fursa za kujikwamua kiuchumi na kuzifanyia kazi fursa hizo kwa maendeleo binafsi na taifa kwa ujumla.

Ni kwa uhalisia huo, ndio maana kwenye maeneo mbalimbali nchini, unaweza kushuhudia maduka yanayouza bidhaa au kutoa huduma zinazofanana yamewekwa mahali pamoja.

Hali hiyo si bahati mbaya, bali hutokea baada ya mmoja kuanza na wengine hufuata kulingana na mwitiko wa wateja wa bidhaa au huduma kwenye eneo husika.

Kanuni hii bila shaka ndio ilitumiwa na mwana Mama, Amina Laizer, mkazi wa Magomeni, Kilosa mkoani Morogoro, ambaye pia ni diwani wa viti maalumu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa.

Simulizi lake kuhusu biashara ya uuzaji wa maziwa, inafanana sana na historia ya Rais mstaafu wa Madagascar, Marc Ravalomanana, ambaye licha ya kwamba amestaafu watu wengi wa taifa hilo bado wanamkumbuka.

Kwa mujibu wa historia, Rais Ravalomanana aliyeitawala Madagascar tangu mwaka 2002 hadi 2009, alipaa kisiasa baada ya kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kwenye ujasinamali wa kuuza maziwa.

Historia hiyo inaonesha kwamba baada ya kumaliza masomo yake yaliyomfikisha hadi Ulaya, alirejea nyumbani kwao katika wilaya ya Manjakandriana na kuamua kuwa mjasiriamali.

Bila kujali usomi wake, inaelezwa kwamba Ravalomanana alikuwa anakusanya maziwa kutoka kwa wafugaji katika eneo hilo, kuyagandisha akishirikiana na mkewe na kisha kuyatembeza mitaani kwa kutumia baiskeli.

Taratibu biashara ilizidi kukua na mwaka 1977, akamudu kutoka kufanyia biashara nyumbani, hadi kufungua duka maalumu la uzalishaji katika eneo linaloitwa Sambaina.

Biashara ilizidi 'kuchanganya' hadi akafungua kiwanda chake cha kwanza cha kusindika maziwa alichokiita Tiko, ambacho kilimpa uwezo wa kuajiri watu watano na kuanza kusambaza maziwa katika jiji la Antananarivo na maeneo mengine.

Katika mkakati wake wa kuboresha uzalishaji maziwa, Ravalomanana aliomba mkopo kutoka Shirika la Maendeleo la Ufaransa (Agence Française de Dévelopment) lakini hakufanikiwa. Hata hivyo, hakukata tamaa.

Alihangaika hadi akapata mkopo wa dola milioni 1.5 mwaka 1982 kupitia Benki ya Dunia (WB) na kuanzisha kampuni ya Tiko ambayo ilikuja kuzaa kampuni zingine kadhaa.

Kampuni ya Tiko ilizidi kukua katika biashara ya mazao yatokanayo na maziwa ikiwemo siagi na jibini na kuanza kusambaza bidhaa zake hadi nje ya Madagascar.

Baadaye Tiko ikaanza pia kujisha na uzalishaji wa juisi, ice cream, mafuta ya kula na soda huku bidhaa zake zikiandikwa 'Vita Malagasy' (Imetengenezwa Madagascar).

Ni kupitia Tiko, jina la Ravalomanana lilikuwa kubwa huku akiajiri maelfu ya watu na hata alipotangaza kugombea urais akaungwa mkono na watu wengi wa ndani na nje ya taifa hilo.

Tukirudi kwa Amina, ambaye pale Kilosa naye ni maarufu kwa biashara ya maziwa, anasema aliamua kujiingiza katika ujasiriamali ili kuongeza kipato cha familia akianza kwa kufanya biashara kadhaa na kisha kugeukia maziwa, biashara inayompa mafanikio makubwa kwa sasa.

"Nilivyoamua kujiingiza kwenye ujasiriamali, biashara yangu ya kwanza ilikuwa ni kukopesha nguo. Baada ya kuona kuna usumbufu katika malipo, nikajaribu biashara ya kutembeza karanga na kukopesha sabuni.

"Kuna mama mmoja wa kimasai, wakati ninapelekea kule biashara zangu, akaniuliza kwa nini nisijaribu biashara ya maziwa? Nilitafakari nikaamua kuifanya," anasema Amina ambaye pia ni Mmasai aliyezaliwa na kukulia mjini.

Diwani huyo anasema alianza kwa kukusanya lita chache za maziwa kutoka kwa wafugaji, akayasindika nyumbani kwake na kisha kuyatembeza katika mitaa ya mji wa Kilosa kwa kutumia baiskeli.

"Nilianza kwa kutembeza lita 10 za maziwa baada ya kuyagandisha na ndani ya miaka miwili, kiasi kiliongezeka hadi kutembeza lita 20 kwa siku.

"Nilikuwa ninakwenda mimi mwenyewe kutafuta maziwa kwa wafugaji kwa kutumia baiskeli, halafu ninayachemsha, ninayagandisha mwenyewe kisha ninafunga kwenye baiskeli na kutembeza mitaani," anasema.

Mjasiriamali huyo anasema kutokana na kutembeza maziwa huku akipita mitaani akinadi maziwa yake kwa wateja, alijikuta akijulikana sana Kilosa kama 'mama maziwa'.

Anasema kwa sasa ana pikipiki mbili anazotumia katika kukusanya na kusambazia maziwa, moja akiendesha yeye mwenyewe.

Mama huyo anasema kulikuwa na uwezekano wa kupanua biashara yake katika kipindi hicho cha miaka miwili, lakini tatizo lilikuwa ni namna ya kupata mtaji ili kununua vifaa vya kusindikia maziwa mengi zaidi.

"Licha ya kutopatikana kirahisi, vifaa vya kusindikia maziwa ni ghali kidogo. Kila nilikoenda kutafuta mtaji ilikuwa ngumu kukopeshwa," anasema.



Amina anasema baada ya kupata udiwani ambao anaamini umetokana na kujulikana kwake kama 'mama maziwa' alifanikiwa kupata mkopo huo benki na kupanua biashara yake.

Mjasiriamali huyo anasema mara ya kwanza alikopa sh. 2,000,000 na kununua vifaa ambavyo hata hivyo alitapeliwa kwa sababu havikufaa kama alivyotarajia.

Anasema alipomaliza mkopo akakopa tena sh milioni tano na kununua keni kadhaa za kugandishia maziwa, pikipiki, friji kubwa, kuchimba kisima cha maji na kujenga visima kwa ajili ya kupozea maziwa.

"Nilikuwa ninasindika lita 10 hadi 20, lakini sasa baada ya kununua vifaa ninasindika wastani wa lita 300," anasema na kuongeza kuwa mpango wake ni kutanua soko hadi Dar es Salaam na Dodoma.

"Mpaka sasa ninasindika mtindi tu, ila kimsingi soko ni kubwa sana hata nikizalisha zaidi ya lita 1,000 soko lipo la uhakika, lakini tatizo ni mtaji ili kununua vifaa vitakavyoniwezesha kuzalisha zaidi na zaidi," alisema.

Anasema anapanga kuwasiliana na Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, aliyewezesha vijana wa Meatu kuanzisha kiwanda cha maziwa ili kujifunza zaidi na kuona namna anavyoweza kumsaidia kufikia malengo yake.

Diwani huyo mwenye mume na watoto wanne, anasema shughuli zake hazimzuii kumhudumia mumewe na watoto huku akiendelea kufanya siasa kwa kuwa shughuli zake zinamkutanisha pia na watu wengi na kusikia matatizo yao.

Kupitia biashara hiyo, anasema amemudu kujenga nyumba Kilosa na Dar es Salaam na kwamba inamwezesha pia kusomesha watoto wake shule za bweni na kuajiri watu saba.

"Pia ninaishi na mabinti wawili wa Kimasai ninaowasomesha. Niliwachukua kwa wazazi wao kwa sababu niliona wanataka kusoma lakini wazazi wao walipanga kuwaozesha," anasema.

Amina anatumia fursa ya makala hii kuwashauri wanawake wenzake kutokata tamaa wanapokuwa wanatafuta na kuwa tayari kufanya"kazi yoyote bila kufikiria kwamba hii ni kazi ya wanaume au ya wanawake.

"Mimi nilikuwa ninatembeza maziwa kwenye baiskeli, tena baiskeli kubwa aina ya Phoenix watu wananishangaa na wala sioni aibu ninapokuwa ninatafuta fedha na ndani ya miaka miwili nilipambana kuendesha baiskeli, jua langu mvua yangu hadi nimefika hapa nilipo," anasema.

Anafafanua kuwa biashara yoyote ina changamoto nyingi na bila uvumilivu, inakushinda, hivyo ni muhimu serikali ikaendelea kutafuta namna ya kuhimiza wafanyabiashara au viwanda kuingiza au kutengeneza vifaa vya kusindikia maziwa ili vipatikane nchini kwa urahisi.

"Ingekuwa vyema kukawa na eneo ambalo mtu ukiwa na pesa yako unakwenda kununua vifaa vya kusindikia maziwa kama unavyonunua bidhaa zingine sokoni. Ninaamini wafanyabiashata wengine pia wanapata shida kama mimi," anasema.

Anashauri pia taasisi za kifedha kama Benki ya Wakulima (TADB), kuwa karibu na wafanyabiashara kama yeye na kuwasaidia namna ya kupata mikopo kwa urahisi au kuwanunulia bidhaa.

Kama ilivyokuwa kwa Rais mstaafu Ravalomanana, simulizi ya diwani Amina inaonesha tunao wajasiriamali wanaoweza kufika mbali kama rais huyo, lakini tatizo ni mitaji, hali inayodhihirika unapofika nyumbani kwa mwanamama huyo mwenye ndoto kubwa ya kushiriki kwenye kuifikia Tanzania ya Viwanda.



Scanned with CamScanner

# TADB yawezesha kiwanda cha nyama milioni 450/-

Na Mwandishi Wetu, Arusha

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina ameipongeza Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini (TADB) kwa kutoa mkopo wa masharti nafuu wa sh. milioni 450 kwa kiwanda cha Meat King Distributors cha Jijini hapa na kuyaomba mabenki mengine yawape wakulima, wavuvi na wafugaji mikopo ya masharti nafuu pia.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea kiwanda hicho akiwa ameambatana na Kaimu Mkurugenzi wa Mikopo wa TADB, Jeremiah Mhada, majuzi, Waziri Mpina, ameeleza kufurahishwa na mkakati wa TADB wa kuinua sekta muhimu za uchumi na kuyaomba mabenki mengine kuunga mkono azma ya serikali ya ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa kuviwezesha viwanda vyenye kufanyakazi kwa ufanisi.

TADB imekipa kiwanda cha Meat King Distributors fedha kuboresha miundombinu ili kuongeza uzalishaji na kwa kununua ng'ombe, mbuzi, kondoo na nguruwe za wafugaji.

Waziri Mpina alisifu juhudi hiyo ya TADB. akisema; "Kuwepo kwa kiwanda cha kusindika nyama kama hiki cha Meat King Distributors ni jambo lenye tija kwa taifa kwa sababu usindikaji unaongeza thamani kwa mazao yanayotokana na mifugo na hivyo kuwanufaisha Watanzania wengi wanaojihusisha na kilimo, uvugaji na uvuvi.

Naomba mabenki yote ya biashara nchini kuiga mfano wa TADB katika kuwezesha wakulima na viwanda kwa kutoa mikopo ya masharti nafuu," alisema Waziri Mpina.

Waziri Mpina alisema wizara yake itaendelea kuunga mkono wawekazaji katika viwanda ambavyo malighafi zake zinategemea mifugo na kusema wizara yake itahimiza ufugaji wa kisasa utakaomfanya mfugaji anufaike zaidi na mifugo yake.

"Tumejipanga kuendelea kutumia wataalamu wa wizara pamoja na wadau wa mifugo kuhakikisha tunakuwa na mifugo bora ambayo itazalisha nyama bora na kuleta ushindani katika soko la ndani na nje ya mipaka ya Tanzania," alisema.

Mhada amesema mkopo huo mpaka sasa umewanufaisha wakulima wadogo 854 ambao wameunganishwa na soko la uhakika linalotakna na kuwepo kwa kiwanda hicho.

"TADB tunakusudia kuleta mageuzi makubwa katika sekta za ufugaji, uvuvi na kilimo ili kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa malighafi hasa katika kipindi hiki ambamo Serikali inatekeleza azma ya ujenzi wa uchumi wa viwanda," alisema na kuongeza kwamba TADB inaunga mkono kiwanda hicho kwa sababu ni taasisi inayowahakikishia wafugaji wa Mkoa Arusha na mikoa ya jirani ajira za moja kwa moja na kukidhi mahitaji yao ya kila siku.

"Kiwanda kimetoa ajira kwa vijana wa Watanzania. Tunaamini mkopo huu utawawezesha vijana wengi zaidi kunufaika na ajira za moja kwa moja kiwandani hapo na zile zitakazotokana na wafugaji wenyewe kwa kuwa watakuwa na uhakika wa soko la mifugo yao," alisema Mhada.

Meat King Distributors ni kiwanda ambacho kinazalisha bidhaa zaidi ya 100 kutokana na malighafi zinzotokana na ng'ombe, mbuzi, kondoo na mazao mengine ya mifugo jambo ambalo limechangia kuwahakikishia wafugaji soko na kuongeza mapato.

Mume adaiwa kumuua mkewe,

mwaka jana, | kubeba hatari ya kuanzisha | Mazingira; Nishati; na Usafirishaji.

HABARI LEO UK 7.

# TADB wapongezwa kwa kukipatia kiwanda mkopo

**Na Mwandishi Wetu, Arusha**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina (pichani) ameipongeza Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini (TADB) kwa kutoa mkopo wa masharti nafuu wa Sh milioni 450 kwa kiwanda cha Meat King Distributors cha Jijini hapa na kuziomba benki nyingine kutoa kwa wakulima, wavuvi na wafugaji mikopo ya masharti nafuu pia.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea kiwanda hicho akiwa ameambatana na Kaimu Mkurugenzi waMikopo wa TADB, Jeremiah Mhada, majuzi, Waziri Mpina, alieleza kufurahishwa na mkakati wa TADB wa kuinua sekta muhimu za uchumi.

Aliziomba benki nyingine kuunga mkono azma ya serikali ya ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa kuviwezesha iwanda vyenye kufanyakazi kwa ufanisi.

TADB imekipa kiwanda cha Meat KingDistributors fedha kuboresha miundombinu ili kuongeza uzalishaji na kwa kununua ng'ombe, mbuzi, kondoo na nguruwe za wafugaji.

"Kuwepo kwa kiwanda cha kusindika nyama kama hiki cha Meat King Distributors ni jambo lenye tija kwa taifa kwasababu usindikaji unaongeza thamani kwa mazao yanayotokana na mifugo na hivyo kuwanufaisha Watanzania wengi wanaojihusisha na kilimo, uvugaji na uvuvi," alieleza.

Mhada alisema mkopo huo mpaka sasa umewanufaisha wakulima wadogo 854 ambao wameunganishwa na soko la uhakika linalotakana na kuwepo kwa kiwanda hicho.

"TADB tunakusudia kuleta mageuzi makubwa katika sekta za ufugaji, uvuvi na kilimo ili kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa malighafi hasa katika kipindi hiki ambacho serikali inatekeleza azma ya ujenzi wa uchumi wa viwanda," alisema.

Alibainisha kuwa kiwanda hicho kimetoa ajira kwa vijana za moja kwa moja na zile zitakazotokana na wafugaji wenyewe.



eja
va
anroads)
gera,
erengera
ifafanua
Katibu
zara ya
kuzi
ano
enzi),
linga
kagua
Rusumo
zara ya

sha
a

a utalii
aliathirika
unda
nu kilicho-
mbalim-
ataalamu
u cha Dar
ya Afya,
Wizara
a Ujenzi,
asiliano,
ya Ndani
TRA kwa
sekta
a kikosi
akata ma-
ywa na
ambapo
li ikoje
imataifa,
a pamoja
ko ya
i gani ya
anya

Scanned with CamScanner

# TADB yakipa kiwanda cha nyama mil. 450/-

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ameipongeza Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini (TADB) kwa kutoa mkopo wa masharti nafuu wa shilingi milioni 450 kwa kiwanda cha Meat King Distributors cha jijini hapa na kuziomba benki nyingine ziwape wakulima, wavuvi na wafugaji mikopo ya masharti nafuu pia.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea kiwanda hicho akiwa ameambatana na Kaimu Mkurugenzi wa Mikopo wa TADB, Jeremiah Mhada, juzi, Waziri Mpina, alieleza kufurahishwa na mkakati wa TADB wa kuinua sekta muhimu za uchumi na kuziomba benki nyingine kuunga mkono azma ya serikali ya ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa kuviwezesha viwanda vyenye kufanyakazi kwa ufanisi.

TADB imekipa kiwanda cha Meat King Distributors fedha kuboresha miundombinu ili kuongeza uzalishaji na kwa kununua ng'ombe, mbuzi, kondoo na nguruwe za wafugaji. Waziri Mpina amesifu juhudi hiyo ya TADB.

"Kuwapo kwa kiwanda cha kusindika nyama kama hiki cha Meat King Distributors ni jambo lenye tija kwa taifa kwa sababu usindikaji unaongeza thamani kwa mazao yanayotokana na mifugo na hivyo kuwanufaisha Watanzania wengi wanaojihusisha na kilimo, ufugaji na uvuvi. Naomba benki zote za biashara nchini kuiga mfano wa TADB katika kuwezesha wakulima na viwanda kwa kutoa mikopo ya masharti nafuu," alisema Waziri Mpina.

Mpina alisema wizara yake itaendelea kuunga mkono wawekazaji katika viwanda ambavyo malighafi zake zinategemea mifugo na kusema wizara yake itahimiza ufugaji wa kisasa utakaomfanya mfugaji anufaike zaidi na mifugo yake.

"Tumejipanga kuendelea kutumia wataalamu wa wizara pamoja na wadau wa mifugo kuhakikisha tunakuwa na mifugo bora ambayo itazalisha nyama bora na kuleta ushindani katika soko la ndani na nje ya mipaka ya Tanzania," alisema.

Mhada alisema mkopo huo mpaka sasa umewanufaisha wakulima wadogo 854 ambao wameunganishwa na soko la uhakika linalotokana na kuwapo kwa kiwanda hicho.

"TADB tunakusudia kuleta mageuzi makubwa katika sekta za ufugaji, uvuvi na kilimo ili kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa malighafi hasa katika kipindi hiki ambamo serikali inatekeleza azma ya ujenzi wa uchumi wa viwanda," alisema na kuongeza kwamba wanaunga mkono kiwanda hicho kwa sababu ni taasisi inayowahakikishia wafugaji wa Mkoa Arusha na mikoa ya jirani ajira za moja kwa moja na kukidhi mahitaji yao ya kila siku.



# Jamii yahamasishwa ufugaji ng'ombe wa maziwa kisasa

**Na MWANDISHI WETU - TANGA**

KIWANDA cha Tanga Fresh, cha jijini Tanga, kinakabiliwa na upungufu mkubwa wa maziwa kutoka kwa wafugaji ambapo Mtendaji Mkuu wa kiwanda hicho, Innocent Mushi, ameitaka jamii kuhakikisha wanageukia ufugaji ili kuongeza uzalishaji wa maziwa kwa wingi nchini.

Hayo aliyasema hivi karibuni mbele ya ujumbe wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), ambapo Mushi aliishukuru TABD kwa kuiwezesha kujenga miundombinu ya kisasa ya kupokea maziwa inayokiwezesha kupokea maziwa yakiwa safi na salama.

"Tumejenga vituo vya kisasa ili kurahisisha ukusanyaji wa maziwa kutoka kwa wafugaji wa maeneo mbali mbali katika jiji la Tanga. Miundombinu hii inasaidia kupunguza upotevu wa maziwa au kuharibika njiani kwani wengi wafugai wanatoka maeneo ya mbali na kiwanda kilipo," alisema Mushi.

Kiongozi huyo alisema Tanga Fresh tayari imenufaisha zaidi ya wafugaji 6,000 kwa kununua maziwa yao katika maeneo mbali mbali mkoani Tanga na mikoa ya jirani ya Kilimanjaro naArusha na pia mikoa mingine ya Morogoro,Mbeya na Njombe. Kwa upande wake wake Mtendaji Mkuu wa Benki ya Kilimo, Japhet Justine, aliuomba Mkoa wa Tanga kuongeza idadi ya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa kwa sababu Tanga Fresh ni soko kubwa la maziwa kwa wafugaji wa Mkoa wa Tanga na mikoa mingine.

"TADB imekopesha vyama viwili vya ushirika ya wafugaji na vinasambaza maziwa kwa wananchi na kukiuzia maziwa Tanga Fresh. Tumo mbioni kuviwesesha vyama 26 ili kuboresha mnyororo wa thamani wa malighafi hii na kuinua mapato ya wafugaji mkoani humu," alisema

Amewaomba wafugaj kuunda vyama vya msingi vya ushirika ili waweze kupata mikopo ya masharti nafuu kutoka TADB na benki za CRDB, NMB, StanicBank.

Scanned with CamScanner

THE GUARDIAN. Page 5.

# * Mpina crusades for local industries, smallholders to be given bank loans

By Guardian Reporter, Arusha

LIVESTOCK and Fisheries minister, Luhaga Mpina has made a passionate appeal to local banks to lend local industries and smallholders in strategic economic sectors, saying if the two were supported fully Tanzania would take-off well as an industrial country.

He made the appeal during a recent visit to Meat King Distributors Company and praised the Tanzania Agricultural Development Bank (TADB) for giving the company a 450m/- soft loan. The loan, he said, enabled the company to buy livestock and fishery products from smallholders in Arusha and neighbouring regions.

The minister was accompanied by TADB Acting Loans Director, Jeremiah Mhanda on his tour of the factory.

"The presence of this factory has great economic significance to our nation because it adds value to agricultural, livestock and fisheries products making many Tanzanians earn a living with ease. I am appealing to our banks to follow the example of the TADB and give smallholders and local industries soft loans that will enable them to grow," he appealed.

He said local industries depended hugely on smallholders for raw materials and because of that inter-dependence, he argued, it was only logical for the banks to support the two parties to enable Tanzania to build a strong industrial base.

Mpina said his ministry would use its own experts and stakeholders to transform the livestock sector so that herders would sell to local industries quality products and earn more from their labour.

Mhada said the loan the TADB gave to the company had benefited 854 smallholder farmers because the factory guaranteed them a permanent ready market for their produce.

"TADB is determined to participate in effecting production reforms in the livestock, fisheries and agricultural sectors that seek to raise production especially now when the government is pushing for establishment of a very strong industrial base," he said adding that TADB was supporting the company because it guaranteed smallholders in Arusha and neighbouring regions a ready and permanent market for their produce.

There was evidence, he said, the bank's loan to the factory would further create direct jobs for more Tanzanian youths and guarantee smallholders a good market for their produce.

Meat King Distributors sells to urban centres, especially cities, 100 different agricultural, meat and fisheries products.

Scanned with CamScanner